

Kanuni za maadili ya wanafunzi

Taarifa kwa wanafunzi na wazazi na walezi.

Katika shule za umma za NSW kila mtu anahisi ni kwake na anajitahidi kufikia viwango vya kujifunza vya juu.

Kanuni hii ni kwa wanafunzi wote wa shule za umma za NSW. Inafaa kwa shughuli zote za shule, ndani na nje ya eneo la shule, zikijumuisha mtandaoni, na jinsi wanafunzi wanavyojiendesha kibinafsi na pamoja na wanafunzi wengine, wafanyakazi wa shule na watu wa jamii.

Nafuata Kanuni kwa kuwa na **heshima, wajibu na usalama**, na kwa kufuata maelekezo ya mwalimu na wafanyakazi.

Heshimu watu wote

Hii ina maana kuwa mwangalifu na mwenye uelewa ili kila mtu ajisikie amekaribishwa na kujumuishwa.

Nitafanya yafuatayo:

- kusikiliza na kusema kwa heshima
- kuwezesha wengine kuangalia kujifunza kwao
- kuthamini na kujumuisha kila mtu na kuwatendea kwa haki
- kutunza mazingira yetu ya shule
- kuvaa sare ya shule sahihi na kwa heshima.

Kuwajibika

Hii ina maana kuwa waangalifu na vitendo vyetu ili kila mtu anaweza kujifunza na kukubaliana.

Nitafanya yafuatayo:

- kuhudhuria shule kila siku ninayoweza, kufika shuleni na darasani kwa wakati, kuleta kile ninachohitaji, na kuwa tayari kujifunza
- kufuata sheria na utaratibu wa shule na darasa
- kutumia teknolojia kwa salama na kwa ajili ya kujifunza
- kukamilisha kazi yangu ya shule, kujaribu kufanya vizuri sana na kuomba msaada wakati ninapohitaji
- kuwasaidia wengine wakati ninapoaweza
- kujifunza kutoka makosa ninayofanya na kujaribu kuboresha.

Kuwa salama

Hii ina maana kijitunza na kuwatunza wengine ili kila mtu aweze kuwa salama katika shule yetu.

Nitafanya yafuatayo:

- kufuata maelekezo ya walimu na wafanyakazi
- kuheshimu nafasi, faragha na vitu vya wengine
- kusema kwa sauti na kuomba msaada ikiwa mtu yeyote anajisikia bila salama au anatendewa isivyo haki
- kutatua tofauti kwa utulivu na haki.

Ili kuwaweka kila mtu salama, lazima nisifanye yafuatayo:

- kutendea mtu yeyote bila haki kwa sababu ya yeye ni nani au kile kinachomfanya awe tofauti na mimi
- kuwa mwenye vurugu, kuumiza, kutishia, kunyanyasa au kumwonea mtu yeyote, ikiwa ni pamoja na kupitia matumizi ya simu, vifaa, kompyuta, mtandaoni au habari ya mtandao wa kijamii
- kuleta silaha, dawa za kulevya haramu, pombe, vape, sigara za kielektroniki au tumbaku shuleni.

Ikiwa nikifanya mambo hayo, wafanyakazi watachukua hatua ili kuwaweka watu wote kwa salama na kuweza kujifunza. Hii inaweza kujumuisha kusimamishwa kwa muda shuleni.

Walimu na wafanyakazi wa shule hunisaidia kujifunza, kufanya chaguzi njema na kukaa salama. Nitafuata sheria, kuwasaidia wengine, kuheshimu haki zao, na kushiriki mawazo yangu kufanya shule yetu kuwa mahali pazuri kujifunza na kuwa sehemu yake.

Natambua kuwa nimepokea Kanuni ya maadili ya wanafunzi na kutambua matarajio yaliyoelezwa.

Jina la mwanafunzi:

Mimi / sisi tunatambua kuwa tumepokea Kanuni ya maadili ya wanafunzi na kutambua matarajio yaliyoelezwa.

Jina la mzazi/mlezi:

Saini ya mzazi/mlezi:

Huduma ya mkalimani ya simu

Ikiwa ungependa kupata taarifa zaidi, tafadhali piga simu kwa mkuu wa shule. Ikiwa unahitaji mkalimani kukusaidia na swali lako, tafadhali piga simu kwa Huduma ya Mkalimani ya Simu kwa 131 450 na omba kupata mkalimani katika lugha yako.

Mwambia mwongozaji wa simu nambari ya simu unayotaka kupigia simu na mwongozaji wa simu atapata mkalimani kwenye simu ili kukusaidia na mazungumzo. Hutatozwa gharama kwa huduma hii.